Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.360
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 29.03.2021; Accepted 01.04.2022; Published on 25.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, M., *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal

# Kuchanganua Aina za Mageuzi katika Maneno ya Sentensi Sahili ya Ekegusii.

**Wilfrida Kemuma.**
**Mount Kenya University, Kenya.**
**Email:** winniekemuma@gmail.com

## IKISIRI

Utafiti huu unachanganua aina za mageuzi zinazojitokeza katika sentensi sahili ya Ekegusii. Utafiti huu ulihasisiwa na nadharia za Sintaksia Finyizi na Sarufi Geuza Maumbo. Data ilikusanywa maktabani kutumia kifaa cha kudondoa data, kupitia kwa vitabu teule vya Ekegusii. Ili kupata sentensi zilizodhihirisha mageuzi, mbinu ya usampulishaji kwa lengo maalum ilitumiwa. Mbinu za maelezo zilitumika katika uwasilishaji wa data. Mchakato hufanywa kwa kufuata kanuni mahsusi zinazoitwa kanuni geuzi. Ugeuzi unafuata utaratibu maalum, haufanywi kiholela. Katika ugeuzi wa maumbo kuna sharti la ukaribu ambapo hakuna kiambajengo kinaweza kuhamishwa zaidi ya fundo funge mbili kutokana na matokeo ya utafiti huu. Kanuni zingine za uhamisho ni kanuni ya ufungami ambapo muundo wa kijenzi kilichofundwa unahitaji uamuliwe na neno tawala linalofaa. Kuna vilele kanuni ya ulafi, kanuni teta na kanuni hamishe. Mwisho kuna kanuni muundo virai, kanuni geuzi na kanuni za mofofonemiki. Utafiti huu unapendekeza kuwa utafiti zaidi unaweza kufanywa kuhusu aina zingine za mageuzi kama vile, geuzi hamishi swalifu, geuzi hamishi la yambwa tendewa katika lugha hii na hata lugha nyinginezo ili kukuza uwanja wa kisintaksia. Kuna uhamisho unaotokea kwa lugha zingine na siyo katika Ekegusii. Hizi pia zinaweza kufanyiwa utafiti. Tafiti zaidi zinaweza kufanyiwa mada hii kwa kutumia nadharia zingine ili kueleza ikiwa kutakuwa na matokeo tofauti.

**Maneno Muhimu:** Sintaksia Finyizi, kiima, kiarifu, kirai.

---***---

**How to cite this article in APA.**

Kemuma, W. (2022). Kuchanganua Aina za Mageuzi katika Maneno ya Sentensi Sahili ya Ekegusii. *Editon Cons. J. Kiswahili*, 4(1), 416-421. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.360

---***---



© 2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.360
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 29.03.2021; Accepted 01.04.2022; Published on 25.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, M., *Editon Cons. J. Kiswahili.* *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

**UTANGULIZI**

Utafiti huu ulijikita katika uchanganuzi wa athari ya mageuzi ya maneno kwenye muundo wa sentensi sahili ya Ekegusii kwa Misingi ya Sintaksia Finyizi na Sarufi Geuza Maumbo. Kwa mujibu wa Chomsky (1965) tuna mageuzi ya aina nyingi. Katika ugeuzi tunapaswa kujua jina la mageuzi, maelezo ya muundo wa sentensi na mabadiliko yanayotokea. Mabadiliko yatokeayo kufuatia mchakato wa ugeuzi ni kama vile udondoshaji, uchopekaji na upanguaji wa vipashio kwenye sentensi. Maelezo haya yanatupa mwanga kuhusu dhana ya mageuzi kwa jumla na kuwa msingi kwetu katika kutalii mageuzi katika lugha ya Ekegusii.

Mageuzi hutawaliwa na kanuni maalumu kulingana na kanuni za Sarufi Bia. Chomsky (1965) anaeleza kuwa kanuni za sehemu msingi huzalisha seti iliyofinywa na mikufu msingi. Mikufu hii ina jukumu la ufafanuzi wa kimuundo unaoitwa kielelezo tungo msingi. Kielelezo tungo huzalisha umbo ndani la sentensi. Huu muundo ndani huelekea kwa kitengo geuza maumbo. Kitengo geuza maumbo hutekeleza mageuzi kama vile kudondoa na kuondoa, kuchopeka, ugeuza maswali, usogezi au uhamishaji wa vipashio na kadhalika. Kitengo geuza maumbo kina aina kadha ya vikwazo vinavyoathiri mageuzi. Radford (1981) anaeleza kuwa sharti la ukaribu linadai kuwa hakuna kiambajengo kinaweza kuhamishwa zaidi ya fundo funge mbili katika utekelezaji wa kanuni yoyote. Kulingana na kanuni za nadharia ya Sarufi Bia, utafiti huu unachunguza ikiwa kanuni hii inaafikiana na zile kanuni zinazotawala mageuzi katika lugha ya Ekegusii.

Kulingana na misingi anuwai iliyowekwa na wataalam kuhusu sarufi, kila lugha ina vikwazo na kanuni zinazofuatwa katika matumizi yake. Baadhi ya kanuni hizi zimeelezwa kuwa bia na husababisha kuwepo kwa miundo mbalimbali ya sentensi katika lugha mbalimbali. Suala la ugeuzaji wa maumbo ya maneno ni msingi mojawapo ambao huathiri miundo ya sentensi. Hivyo basi utafiti huu unanuia kuchanganua mageuzi ya maneno katika sentensi sahili ya Ekegusii na kubainisha kanuni zinazotawala mageuzi hayo.Kwa misingi ya tafiti za awali katika lugha nyinginezo, utafiti huu unajaza pengo la kufafanua mageuzi ya maneno katika sentensi sahili ya Ekegusii kama msingi muhimu wa kuelezea sarufi ya lugha hii.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

Mageuzi ya maneno katika sentensi huathiriwa na kauli kwani hatuwezi kuzungumzia mageuzi bila kushughulikia dhana ya kauli. Kwa mujibu wa Massamba na wenzake (1999) dhana ya kauli katika sarufi kuhusu uhusiano uliopo baina ya ama kitenzi na kiima au kitenzi, kiima na yambwa. Kwa ufupi dhana hii inahusu mtenda na mtendwa katika sentensi. Kagwa na wenzake (2013) wameigawa dhana ya kauli katika aina kuu mbili ambazo ni kauli ya kutenda na kauli ya kutendwa. Kauli ya kutenda hudhihirisha kwamba kiima katika sentensi inayohusika ina uamilifu wa kutenda jambo. Katika sentensi tenda yambwa huathirika kwa namna fulani. Kuathirika huku ni kwa namna ya kufanyiwa mageuzi ambapo viambajengo hudondoshwa, huchopekwa, ilhali vingine vikihamishwa.

Kauli ya kutendewa inaashiria kuwa kiima kina uamilifu wa kutendwa, yaani kiima kinafanyiwa tendo fulani. Sentensi tenda na tendwa zinahusiana pakubwa. Uhusiano huu unajitokeza baina ya kiima, kitenzi na yambwa katika makundi yote mawili ya sentensi. Kitenzi kinaonekana kuwa kiini cha uhusiano huo kwa sababu kinahusisha mtenda na mtendwa. Tofauti zilizoko ni za kimuundo tu. Katika sentensi tenda, kiima kinachukua uamilifu wa mtenda na yambwa inachukua uamilifu wa mtendwa. Kwa hivyo mageuzi hutokea katika kauli ya tendwa.

Dhana ya kauli ni muhimu katika utafiti huu. kwani iliwezesha kubaini ni mambo yapi hufanyikia sentensi katika hali ya mageuzi. Dhana hii ilisaidia kubaini pia ni viambajengo gani huingizwa katika sentensi za kauli mbalimbali na ni zipi huondoshwa mbali na kuwezesha



© 2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.360
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 29.03.2021; Accepted 01.04.2022; Published on 25.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, M., *Editon Cons. J. Kiswahili*. *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

ISSN: 2663-9289

kutambua vile viambishi vinavyopachikwa katika kauli mbalimbali. Utafiti ulijikita katika kauli hizi mbili kwani ndizo zinazopatikana sana sana katika sentensi sahili ambayo ndiyo eneo la utafiti wetu. Kauli zingine kama vile za kurejelea, kutendana, kutendeka na kadhalika haziingiliani sana na eneo la utafiti huu. Katika kubainisha dhana ya kauli, utafiti huu ulibidi vilevile uangalie dhana ya sarufi geuzi na sarufi zalishi. Sentensi ni kipashio kikubwa cha kimuundo chenye maana kamili (Massamba na wengine, 1999). Miundo ya sentensi uhusisha vipashio vingine vidogo kimiundo. Vipashio hivyo ni virai na vishazi.

Kazi ya waandishi hawa imekuwa na mashiko makubwa katika utafiti wetu kwa sababu viambajengo vya sentensi vilivyotajwa na wataalamu ndivyo vimekuwa nguzo za utafiti wetu kwa jumla. Mbali na hayo imetufaa katika kazi hii kwa sababu imetuwezesha kubaini viambajengo vya sentensi. Hali kadhalika kazi yao imerahisisha utafiti huu kwa jumla na pia kuangazia viambishi vinavyopachikwa kwenye mzizi wa neno mbali na kushughulikia dhana ya upatanishi wa kisarufi katika sentensi. Sifa hizi mahsusi zinazojadiliwa zina umuhimu wake katika dhana ya uchanganuzi wa sentensi sahihi ya Ekegusii.

## MATOKEO YA UTAFITI

### Aina za Mageuzi

Kitengo cha sintaksia huhusu vitengo viwili; kijitengo msingi ambacho hushughulikia sheria za kuunda virai katika sentensi na pili kijitengo geuzi. Hiki cha pili ndicho cha muhimu katika mada yetu ya sasa. Kijitengo geuzi huonyesha jinsi ya kugeuza sentensi kutoka muundo mmoja hadi mwingine. Kama tulivyoona hapo awali, sentensi zinapogeuzwa huwa kunatokea mabadiliko kama vile kudondoshwa kwa elementi, kuongezwa elementi na kupanguliwa kwa elementi katika sentensi fulani. Wanaisimu kama vile Bornstein (1978) na Haegemen (1991) wameyainisha mageuzi katika makundi mawili makuu-yale ya shuruti na yale ya hiari. Aidha, mageuzi yanaweza kuainishwa kwa mujibu wa kategoria za maneno zinazohusika. Kutokana na haya, geuzi linaweza kuwa la jumla ambalo huathiri tungo nzima au likawa geuzi kuhusu kategoria mahsusi kama vile kuhusu kiima (KN) au Kitenzi (T). Katika kushughulikia sentensi sahili aina moja ya mageuzi hujitokeza kwa mujibu wa utafiti huu-geuzi tendwi.

### Geuzi Tendwi.

Haegemen (1991) amelifanya geuzi hili kuwa ni la uhamishi kwa sababu linahusisha uhamishaji wa baadhi ya vipashio kwa kubadilisha nafasi inayokaliwa na vipashio hivyo katika kategoria za kiima na yambwa/shamirisho. Geuzi hili linahusisha upangaji upya wa virai nomino katika tungo pamoja na kuingizwa kwa kihusishi "*na*" Kanuni geuzi tendwa. Pia hufanya kazi ya kuigeuza sentensi tendi na kuifanya tendwa kwa mfano:

| **Tendi** | **Tendwa** |
|---|---|
| (1) *Kwana* sema | *Kwanwa* semwa |
| (2) *Ruga* Pika | *Rugwa* Pikwa |
| (3) *Tera* Imba | *Terwa* Imbwa |

**Tendi** **Tendwa**
(4) *Omwenga ororire Nyakundi* *Nyakundi ororirwe na Omwenga*
Omwenga amemwona Nyakundi
Nyakundi ameonwa na Omwenga

Kwa mujibu wa Haegemen na kama inavyodhihirika katika mifano ya sentensi hizi, utendi una sifa kadha za kisintaksia.

Sifa hizi ni pamoja na:

1. Kitenzi kuathirika kimofolojia
2. Uhamisho wa kirai nomino ni wa kishuruti.
3. Kirai Nomino kina dhima ya uhusika
4. Uhamishaji wa Kirai nomino unakubalika kwa sababu nafasi ya kiima katika geuzi tendwi i wazi. Kila sentensi inahusishwa na viwango viwili vya uwasilishwaji wa kisintaksia-umbo la ndani na umbo la nje. Maneno mbalimbali katika sentensi huwa na dhima ya uhusika. Uhusika huashiria uhusiano wa kisemantiki kati ya maneno na vitenzi katika sentensi. Kwa mfano



© 2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

# Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.360
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 29.03.2021; Accepted 01.04.2022; Published on 25.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, M., *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal

kitenzi *rora* ona kina uhusika wa aina mbili kwanza kuna uhusika wa kubainisha dhima ya mtenda kwa kiima. Pili, kinatambulisha dhima ya mtendwa katika taarifa. Uhusika huu ni muhimu sana katika geuzi tendwi kwa sababu geuzi tendwi linaweza kufanyika tu ikiwa sentensi ina virai niomino viwili (Kiima na yambwa tendwa) pamoja na kitenzi kielekezi kwa mfano

(5) (a) *Omwenga ororire Nyakundi*
Omwenga amemwona Nyakundi
(b) *Nyakundi ororirwe na Omwenga*
Nyakundi ameonwa na Omwenga

Sentensi (a) na (b) zina maana sawa ingawa miundo yao ni tofauti. Tofauti hii imetokana na mageuzi fulani yaliyofanyiwa vikundi nomino na kitenzi. Kitenzi kimefanyiwa mageuzi ya kimofolojia *ororire – ororirwe*. Kihusishi {na} kimechopekwa katika sentensi tendwa. Sentensi tenda na tendwa huwa na uhusiano kwa sababu zote mbili huanza katika muundo wa ndani unaofanana. Miundo ya nje ya sentensi tendi na sentensi tendwa ndiyo hutofautiana. Ili kupata sentensi tendi, kanuni za kimofolojia za upatanishi wa kiima na kiarifu na uambishaji wa kiwakilishi wakati hutumika kwenye kitenzi. Sentensi inayopatikana kwa namna hiyo ni sentensi tendi ambayo huwa ni sentensi ya msingi na ndiyo msingi wa kanuni muundo virai. Ili kupata sentensi tendwi mageuzi muhimu hufanyika katika muundo wa nje. Mageuzi hayo huletwa na kanuni geuzi la utendwa. Sentensi tendi ya Ekegusii huwa ni yakanifu.

Mfano wa sentensi tendi kutokana na mfano wa (a) hapo juu ni:

*Omwenga ororire Nyakundi* (Tungo Tendi)
S ⟶ KN - T - KN2

Huu muundo wa KN1 - T - KN2 ndio unaofanyiwa mageuzi ya uhamishi na kubadilisha nafasi kati ya KN1 na KN2 na kuingiza kihusishi {na} kati ya kitenzi na Kirai nomino cha kiima. Mageuzi haya yanaweza kuwasilishwa hivi:

S ⟶ KN1 T KN2 = KN2 T {na} KN1. Alama = inaonyesha mabadiliko au athari katika muundo wa sentensi iliyopitia mageuzi. Kanuni hii ya mageuzi inazalisha utungo ufuatao unaoonyesha uhamishaji wa mpangilio wa vikundi nomino pamoja na kuchopekwa kwa kihusishi {na}.

*Nyakundi rora na Omwenga*
KN2 T H KN1

Muundo huu haujakamilika na kwa hivyo kanuni za kimofolojia zinahitajika kuukamilisha. Katika mageuzi haya KN ndicho kiima kinachotawala upatanishi wa kitenzi. Mchakato huu wa mageuzi unazua mambo yafuatayo katika muundo wa sentensi tendwi:

1. KN kinaambatinisha mofimu ya upatanishi katika kitenzi
2. Mofu ya kauli ya tendwi {w} huambishwa kwenye kitenzi baada ya shina la kitenzi
3. Uambishaji kwenye kitenzi unakifanya kuwa na muundo wa kipatanishi kinachofuatwa na kiwakati, shina ambalo huambishwa kiambishi kiendelezi na kiishio. Kielezo cha mageuzi haya ni:

   Kitenzi T ⟶ Kipatanishi + kiwakati +Shina (Tendwi) + Kiishio

   Matokeo ya kanuni hizi ni sentensi tendwi yenye muundo huu:

   *Nyakundi ororirwe na omwenga*.


   Uhusiano wa sentensi hizi mbili tendi na tendwi umefanikishwa kwa kutumia muundo kirai na kanuni geuzi za kimofolojia. Tungo tendi zote kwa hivyo huwa na muundo wa S ⟶ KN1 T KN2, ilhali sentensi tendwi huwa na muundo wa S ⟶ KN2 T (Tendwi) {na} KN1.

   Kielelezo tungo cha sentensi tendi
   Uwakilishi wa mchoro matawi
   *Omwenga Ororire Nyakundi*




© 2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)
DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.360
ISSN: 2663-9289
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
Received: 29.03.2021; Accepted 01.04.2022; Published on 25.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, M., *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal




**Mchoro 1: Mchoro wa Sentensi Tendi**

Kielelezo cha sentensi tendwi




**Mchoro 2: Mchoro wa Sentensi Tendwi**

Geuzi tendwi huhamisha nafasi za kirai nomino cha kiima na kile cha yambwa au shamirisho kwa kubadilisha nafasi na kusababisha mabadiliko ya kimuundo. Geuzi tendwi vile vile linaweza kuwa sentensi inayosheheni yambwa tendwa na yambwa tendewa. Sentensi hizi huwa na nomino mbili na hujumuisha virai nomino vitatu. Ili kutekeleza mageuzi tendwi katika sentensi zenye muundo huu kila moja ya virai hivyo ni lazima vihamishwe, pamoja na uchopekaji wa kihusishi {na}.

Mfano katika sentensi:

(6) (a) *Ng'ina agatachera omwana oye amache amarabu.*

Mama alimchotea mtoto wake maji safi

(b) *Omwana agatacherwa amache amarabu na ng'ina*

Mtoto alichotewa maji safi na mama yake.

Sentensi ya (a) ni tendi na (b) ni tendwi.

Muundo wa sentensi tendi hii ni $S \longrightarrow KN_1 T KN_2 V KN3V$ nayo kanuni ya muundo virai ya sentensi tendwi ni :

$S \longrightarrow KN_2\ T\ KN_3 V$ na $KN_1 V$

Ikiwa sentensi (a) itachukuliwa kama sentensi ya msingi kwa mujibu wa kanuni ya miundo virai basi muundo wa sentensi tendwi inayoonyesha shamirisho mbili itakuwa hivi:

$S \longrightarrow KN_1 T\ KN2_{KN3}\ KN_2\ TKN3\ KN1$

Kwa mujibu wa kanuni hii KN cha kiima huchukua nafasi ya KN cha kitendwa huku KN cha kitendwa kikihamishwa hadi nafasi ya KN kitendewa. Geuzi hili huathiri mpangilio wa yambwa hizi katika sentensi inayobeba aina mbili za yambwa. Yambwa tenda aghalabu hutokea kabla ya yambwa tendwa.

**Geuzi Hamishi**

Geuzi hamishi linasawiana na geuzi tendwi katika uhamishaji wa viambajengo vya sentensi, jambo ambalo husababisha athari katika mpangilio wa maneno katika sentensi. Tofauti kuu kati ya geuzi tendwi na geuzi hamishi ni kuwa kitenzi katika geuzi hamishi hakibadilishi umbo



© 2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.360
Volume: 04 Issue: 01 | April-2022|
ISSN: 2663-9289
Received: 29.03.2021; Accepted 01.04.2022; Published on 25.04. 2022 at www.editoncpublishing.org
Kemuma, M., *Editon Cons. J. Kiswahili.* Double –Blind Peer Reviewed Journal

lake. Pili ni kuwa katika geuzi hamishi kihusishi hakichopekwi katika sentensi iliyofanyiwa mageuzi. Katika aina hii ya geuzi nafasi inayokaliwa na nomino hubadilishwa na hivyo kuleta miundo mbalimbali ya nje ya muundo mmoja wa ndani.

Mfano katika sentensi:

(7) a.)*Abana bakairana getii*
Watoto walirudi uwanjani
b.)*Getii abana bakairana*
Uwanjani watoto walirudi
c.) *Bakairana getii abana*
Walirudi uwanjani watoto

Katika mfano huu wa sentensi 7, sentensi (b) na (c) ni maumbo tofauti ya sentensi (a). Vipashio katika hizi sentensi tatu zinaweza kubadilishana nafasi lakini maana ya tungo haibadiliki kwani hayo ni maumbo tofauti ya muundo mmoja wa ndani.

Uhusiano baina ya sentensi hii hujibainisha hivi kimaumbo:

Abana bakairana getii → Getii abana bakairana
S → KNT T KN2 KN$_2$ KN1 T
Uhusiano baina ya (a) na (c) ni:
Abana bakairana getii → Bakairana getii abana.
S → KN$_1$ T KN$_2$ T KN2 KN$_1$

Kwa mujibu wa Haegeman (1991) geuzi hamishi ina sifa ya kuhifadhi muundo wa ndani katika kiwango cha muundo wa nje.

## MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Mahitimisho:** Mchakato hufanywa kwa kufuata kanuni mahsusi zinazoitwa kanuni geuzi. Ugeuzi unafuata utaratibu maalum, haufanywi kiholela. Katika ugeuzi wa maumbo kuna sharti la ukaribu ambapo hakuna kiambajengo kinaweza kuhamishwa zaidi ya fundo funge mbili kutokana na matokeo ya utafiti huu. Kanuni zingine za uhamisho ni kanuni ya ufungami ambapo muundo wa kijenzi kilichofundwa unahitaji uamuliwe na neno tawala linalofaa. Kuna vilele kanuni ya ulafi, kanuni teta na kanuni hamishe. Mwisho kuna kanuni muundo virai, kanuni geuzi na kanuni za mofofonemiki.

**Mapendekezo**: Utafiti zaidi unaweza kufanywa kuhusu aina zingine za mageuzi kama vile, geuzi hamishi swalifu, geuzi hamishi la yambwa tendewa katika lugha hii na hata lugha nyinginezo ili kukuza uwanja wa kisintaksia. Kuna uhamisho unaotokea kwa lugha zingine na siyo katika Ekegusii. Hizi pia zinaweza kufanyiwa utafiti.

## MAREJELEO

Bornstein, D. (1978). *An Introduction to Transformational Grammar*. Winthrop Publishers.
Chomsky, N. (1965). *Aspects of the Theory of Syntax*. Massachuessette Institute of Technology Press.
Kagwa, F. M., Kombo, K., & Waihiga, G. (2013). *Kioo Cha K.C.S.E. Kiswahili*. Spotlight Publishers (EA) Limited.
Massamba, D. P. B., Kihore, Y.M., & Hokororo, J. I. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu.*TUKI.



© 2022, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non-Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org